GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. **247** Rajab-Shaban **1446** AH Januari– **2025** Sulhu **1404** HS BEI TSH 800/=

Jalsa ya Mkoa wa Morogoro Yafana

Na. Sh. Karim Ud Din Shamsi



Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya, alianzisha utaratibu wa kufanya Jalsa (mkutano) kwa lengo la kuwalea wanajumuiya. Kwa kushiriki katika Jalsa wanapata kujisafisha vizuri na kutakasa khulka, tabia na roho zao. Safari moja alisema Jalsa ni chanzo muhimu cha maendeleo ya kiroho; naye alifanya maombi makhsusi kwa ajili ya washiriki. Watu 75 walihudhuria katika Jalsa ya kwanza iliyofanyika Qadian, India.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, siku hizi kila nchi inafanya mkutano wake wa mwaka uitwao Jalsa Salana. Jalsa Salana za baadhi ya nchi hurushwa kupitia Muslim Television Ahmadiyya (MTA) na watu wengi duniani wanashiriki kwa kufuatilia matangazo yake kwenye setilaiti, intaneti na mitandao ya kijamii. Mikutano hii inadhihirisha ukweli wa Hazrat Ahmad[as] kwani baraka zake zimeanza kupatikana katika mataifa mengi duniani na watu wengi wanafaidi kwake. Kwa kufuatia Jalsa Salana iliyofanyika hapa nchini Tanzania mwezi wa Septemba mwaka 2024, mikutano mingine inaandaliwa katika ngazi ya mikoa. Lengo na makusudio kuwa ni kutoa nafasi kwa wanajumuiya wengi kushiriki na kufaidika na mawaidha na kujipatia malezi ya kiroho. Hivyo, Jalsa ya Mkoa wa Morogoro ilifanyika Jumamosi tarehe 14, Disemba 2024.

Kwa ajili ya Jalsa ya mkoa kamati kadhaa za maandalizi ziliundwa ambazo ni Kamati ya Mwaliko, Kamati ya Mapokezi, Kamati ya Usafi, Kamati ya Chakula na Kamati ya Ukumbi na Mapambo.

Jamia Ahmadiyya Kihonda, Morogoro iliamuliwa kuwa ni eneo la Jalsa ya mkoa. Mkuu wa Chuo cha Jamia alipelekwa ombi la kufanya Jalsa katika ukumbi wa Jamia uitwao "Masroor Hall" na akatoa ruhusa. Mgeni rasmi wa Jalsa hii alikuwa Mheshimiwa Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad. Yeye alikubali ombi letu na akaja Morogoro pamoja na msafara wake.

Pia, wanajumuiya wengine wakiongozana na Sadr Majlis Ansarullah na Sadr Majlis Khuddam ul Ahmadiyya walifunga safari kushiriki katika Jalsa hii. Mwenyezi Mungu Awalipe malipo mema. Aamin

Siku ya Jalsa ilianza na Tahajjud (Sala ya Usiku).

Amir na Mbashiri Mkuu aliongoza Sala hii pamoja na Sala ya Alfajiri kisha darsa ya Kurani Tukufu ilitolewa na Sheikh wa Mkoa.

Jalsa ya mkoa ilikuwa na vikao viwili. Kikao cha kwanza kilifunguliwa asubuhi na Amir na Mbashiri Mkuu. Yeye alitoa hotuba ya ufunguzi na akaongoza maombi ya pamoja. Baada ya hapo hotuba nyingine zilitolewa. Hotuba ya kwanza ilitolewa na Sheikh Abdurrahman Ame (Naibu Amir) juu ya

UK. 03

Ujumbe wa Huzur Aqdas[atba] kufuatia Ijtimaa ya Ansarullah Tanzania

UK. 04

HERI YA MWAKA MPYA

>UK .02

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SULUHU HUDAIBIYAH

Tukio ambalo Allah ameliita ni "ushindi ulio dhahiri", ni tukio ambalo tunatakiwa tufahamu chimbuko lake, tulisome, tutafakari, tudadisi kwani bila wasiwasi wowote kuna somo kubwa kwa ajili ya ulimwengu ulioghubikwa na mateso ya kila aina.

Mwaka wa sita Al-Hijra Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alipata njozi akiingia maka na kufanya ibada ya Umrah. Mtume[saw] na masahaba walifunga safari kwenda kufanya umrah. Mahala paitwapo Hudaibiyah, Makureish hawakuwaruhusu waingie Maka. Jambo hili lilileta mfadhaiko mkubwa. Hatimae yalifanyika makubaliano ambayo Historia inayaita suluh Hudaibiyah. Kwa jicho la kawaida yalikuwa ni makubaliano yaliyowaumiza baadhi ya Masahaba.

Mwanzoni tu mwa kuandika mkataba huo yalijitokeza matatizo yaliyohitaji Mtume wa Mwenyezi Mungu pekee kuyatatua.

Mwandishi alikuwa Seyidna Ali[ra] na akaandika Bismillahi Rahman Rahim lakini Suhail bin Amir akakataa kata kata na kusema hakujua lolote kuhusu Ar-Rahman, alisisitiza iandikwe Bi-Ismika Allahumma (katika jina lako Allah) Mtume wa Allah akakubali na walipofika kwenye makubaliano baina ya Muhammad Rasulullah, Suhail alipinga tena na kusema tungeamini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu tusingekukataza kuingia Maka.

Mtukufu Mtume[saw] akakubali na masharti yenyewe yalikuwa,

1) Waislam watarudi kwa hivi sasa na watarejea kufanya umrah mwaka ujao, wanaweza kuja na majambia lakini wawe wameyaweka katika ara.

2) Vita itasimama kwa muda wa miaka kumi na hakuna upande utakaoshika silaha

3) Anayetaka kufanya mapatano na Muhammad[saw] anaruhusiwa na Makureish wanaruhusiwa kufanya mapatano na watu wowote wengine.

4) Mtu yeyote kutoka kwa Makureshi akienda kwa Muhammad[saw] bila ya ruhusa ya mlinzi wake arudishwe kwa Makureshi na wafuasi wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] wakienda kwa Makureshi wasirudishwe Madina. Mapatano yeyote, makubaliano yoyote yanahitaji maombi na kutegemea Allah. Unaweza kupenda kitu kumbe kikawa na madhara kwako na ukachukia kitu kumbe kina heri kwako. Kufika katika uamuzi wa namna hiyo unahitaji msaada wa Allah. Na maisha yote ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw] hakufanya jambo lolote bila maombi.

Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikuwa mwana diplomasia wa kiwango cha juu. Alielewa kwamba katika makubaliano yoyote lazima uwe tayari kupoteza baadhi ya vitu ilimradi shabaha yako ya msingi haijapotea. Siku zote alishika njia ya kati bila kung'ang'ania pale pale na hayo ndiyo mafundisho ya Islam kuchukua njia ya kati. Kama maji hayapatikani uchukue tayamamu. Mtukufu Mtume_Muhammad[saw] kwa sababu ya amani na utengamano alikuwa tayari kukubali masharti makali na magumu ya makureishi. Wao walisema wanafanya mkataba na Muhammad bin Abdallah na sio Muhammad Rasullah.

Seyidna Ali[ra] aliona muhali kufuta maneno hayo. Mtukufu Mtume Muhammad[saw] akaoneshwa maneno hayo yalipo na akayafuta. Nia ya safari yake ilikuwa kufanya umrah, makureshi wakasema itakuwa mwakani sio mwaka huu. Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikubali sharti hilo ingawaje liliwapa jakamoyo masahaba.

Kwa ujumla Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikuwa anaona kwa nuru ya Allah. Aliweza kuona mahali pa mbali ambapo wengine hawakuona. Historia ya Islam inaonesha kwamba hakuna kipindi cha utulivu, mahubiri na amani kama kile kipindi cha amani baina ya waislam na makureshi. Ni kipindi Islam ilipopiga hatua kubwa katika kueneza Tauhid. Wafalme walifikishiwa ujumbe na watu wa kawaida pia.

Na suluhu ya Hudaibiyah inawasuta wale wanaotoa masingizio ya kwamba dini ya Islam ilienezwa kwa upanga. Masingizio haya hayana msaada wowote wa Historia. Hatujawahi kutajiwa hata mtu mmoja ambaye ameingizwa katika Islam kwa njia ya kulazimishwa au kwa upanga. Ushahidi tulionao ni kwamba Mtukufu Mtume Muhammad[saw] katika vita moja alimkasirikia sahaba ambaye licha ya adui kutoa shahada alimuuwa na Mtukufu Mtume Muhammad[saw] akamuuliza, kama ametoa Shahada hiyo kwa woga, wewe umeingia katika roho yake?, sahaba yule alisikitika na daima aliendelea kuomba ili asamehewe. Balozi mmoja alitumwa na nchi yake kuja Madina kuonana na Mtukufu Mtume Muhammad[saw] kipindi alichokaa Madina aliathirika na kusema anabaki na kujiunga na Islam. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alikataa na alimwambia aende na kama bado ana imani afunge safari mahsusi kwa ajili ya kuingia katika Islam.

Mtukufu Mtume Muhammad[saw] aliwapokea wale tu walioelewa barabara mafundisho ya Islam.

Tizama Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alivyokuwa mtu aliyeheshimu mapatano. Wakati makubaliano yanafikia ukingoni aliletwa Abu Jadal ambaye alikuwa amefungwa minyororo na amejeruhiwa. Aliomba asirudishwe Maka lakini Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alimuambia amtegemee Allah kwani asingeweza kuvunja ahadi.

Suluhu ya Hudaibiya ni alama kubwa ya kwamba Mtukufu Mtume Muhammadkwani ni mfanohakutaka vita, alitaka amani. Kama alikuwa mtu wa vita na mwenye nia ya kueneza Islam kwa upanga asingekubaliana na masharti ya Hudaibiya. Maadui wa Islam wasome vizuri mapatano ya Hudaibiya, kwani ni mfano unaong'ara wakuelewa msimamo wa Mtukufu Mtume Muhammadkwani ni mfano na kutoa ushahidi wa kutosha kuwa yeye ni rehema kwa walimwengu.



QUR'AN TUKUFU

9. Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao. *Al-Mu'Minuun 23:09*

وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ۝٩



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu raia wake. Amiri ni mchungaji. Na mtu ni mchungaji wa watu wa nyumbani mwake. Na mwanamke ni mchungaji wa nyumba ya mumewe na watoto wake. Basi kila mmoja ni mchungaji na kila mmoja ataulizwa kuhusu raia wake. (Bukhari)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Tafsiri na maelezo ya Hazrat Masihe Maud[a.s]:
Waaminio ni wale ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao yaani hawaachi dakika yoyote ya taqwa na ya uaangalifu juu ya kutekeleza ahadi na amana zao.(Zamima Barahine Ahmadiya,Juzu 5,R.Kh.J.21 uk 239-240)

Bodi ya Uhariri wa Gazeti la Mapenzi Ya Mungu inawatakia heri ya mwaka mpya wa 2025. Tunamuomba Allah aufanye mwaka wa 2025 wenye baraka na fanaka tele. A m i n

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga 2. Mahmood Hamsin Mubiru. 3. Sheikh Shahab Ahmad. 4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Jalsa ya Mkoa wa Morogoro Yafana

Kutoka uk. 01



mada "Wajibu wa Wanandoa".

Hotuba ya Pili ilitolewa na Sheikh Abid Mahmood (Naib Amir na Principal Jamia) kuhusu "Ahadi ya Bai'ati na majukumu ya Mwahmadiya". Hotuba ya tatu ilitolewa na Sheikh Karim-ud-din Shams juu ya "Wajibu wetu wa kudumisha nidhamu ya Ukhalifu". Hapo ndipo kikao cha kwanza cha Jalsa ya mkoa kilimalizika majira ya saa saba mchana. Sala ya Adhuhuri na Alasiri zilisaliwa kwa kuchanganya saa saba na robo na washiriki wote walipewa chakula cha mchana.

Kikao cha pili kilianza saa nane na nusu. Kikao hiki kilisimamiwa na viongozi wa Tanzim ambapo wanatazim walipewa miongozo mbalimbali kuhusiana na majukumu yao. Baada ya hapo wageni waalikwa wakiwemo viongozi wa serikali na viongozi wa dini walipewa nafasi ya kutoa salamu zao. Miongoni mwao alikuwa Askofu wa Kanisa la Anglikana Bw. Godfrey Hadadi Sehaba.

Yeye alimwakilisha mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano ya Mkoa. Askofu huyu alipewa zawadi ya Kurani Tukufu na akapokea kwa furaha kubwa sana.

Kisha Mchungaji Regnard Heron Mdugi alipewa zawadi ya kitabu cha "Revelation, Rationality, Knowledge, and Truth. Halafu Sheikh Alhaj Korofeti wa dhehebu la Shia pia alipewa Kurani Tukufu. Mheshimiwa diwani na viongozi wengine wa serikali pia walipewa zawadi ya vitabu vya Jamaat. Hotuba ya kufunga kikao hiki ilitolewa na Amir na Mbashiri Mkuu. Hotuba hii ilijaa elimu, maarifa na utamu wa kipekee na Jalsa ya mkoa ilimalizika kwa kufanya maombi ya pamoja.

Baada ya hapo Sheikh wa Mkoa aliwakaribisha wageni waalikwa nyumbani kwake kupata chai na vitafunwa. Fursa hii ilitumika kuwatambulisha zaidi kuhusu Jamaat.

Hafla ya Kumwaga Sheikh wa Mkoa wa Morogoro kwa mujibu wa mwongozo wa Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Karim-ud din Shams alipata uhamisho kwenda Dodoma na Sheikh Daud Ahmad Bhatti alipangiwa kuja Morogoro kuchukua nafasi yake ya Sheikh wa Mkoa. Hafla ya kumwaga Sheikh wa Mkoa anayeondoka na kumkaribisha Sheikh mpya anayeingia ilifanyika baada ya kusali Sala ya Magharib na Isha.

Hafla hii ilianza na usomaji wa Kurani Tukufu. Amir na Mbashiri Mkuu alikuwa mgeni rasmi. Rais wa Mkoa Bw. Mussa Kasita alipewa nafasi ya kumwaga Sheikh Karim ud Din na kumkaribisha Sheikh Daud Ahmad Bhatti. Alieleza baadhi ya majukumu aliyoyatekeleza Sheikh Karim ud Din katika muda wake wa kufanya kazi katika mkoa huu. Kisha Sheikh Abid Mahmood (Naib Amir na Principal Jamia) alieleza kuhusu kipindi alichokaa Sheikh anayeondoka na alimkaribisha sheikh mpya. Baada yake Sheikh Daud Ahmad Bhatti aliwatolea shukurani washiriki wote kwa makaribisho mazuri. Halafu Amir na Mbashiri Mkuu alifunga kikao hiki kwa nasaha maalum. Sheikh Karim ud din alipewa zawadi ya koti na zawadi nyingine kwa ajili ya mke wake. Zawadi hizi zilitolewa na wanajumuiya wa Morogoro mjini.

Huduma ya Dar uz Ziafat huduma ya kuwakarimu wageni wa Jalsa ya mkoa ilianza siku ya Ijumaa ambapo watu walipewa chakula cha jioni. Huduma hii iliendelea hadi chai ya asubuhi siku ya Jumapili na wageni wengi walifurahi kwa kila walichokipata.

Mafanikio ya Jalsa hiyo yalikuwa Kwa ajili ya dua Maalum ya Khalifa wetu Mpendwa Kwa sababu Jalsa hii ilikuwa ni sehemu ya ziara ya Amiri na Mbashiri Mkuu katika mkoa wetu. Amir sahib alimwandikia Hazrat Amirul Muminiin barua ya kupata maombi yake maalumu kuhusu ziara kwa jumla. Hali ya hewa kabla ya ziara ilikuwa haitulii kabisa kwa sababu ya mvua kubwa lakini tuliona muujiza kwamba katika siku zote za ziara hii mvua hazikuathiri hata kidogo na safari zote zilifanyika kwa mafanikio makubwa. Alhamdu Lillah.

Shukrani nyingi zinapaswa kutolewa kwa Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya Tanzania na timu yake. Walijitolea sana katika kufanya maadalizi ya Jalsa ya mkoa. Pia, shukrani ziwaendee wageni wote walioshiriki katika Jalsa hii. Mwenyezi Mungu awalipe wote Malipo Mema. Jazakumullah Ahsanul Jazaa. Mahudhurio ya Jalsa yalikuwa 356 wakiwemo waahmadiyya wapya wa kitongoji cha Kanitangaze, Mikese na baadhi ya majirani wasiokuwa Waahmadiyya.

Tunamwomba Allah kuwa juhudi hizo zizae matunda mema na makubwa. Aamin.

TANGAZO

UONGOZI WA LAJNA IMAILLAH TANZANIA UNAWATANGAZIA LAJNA NA NASRAT WOTE NCHINI KUWA IJTIMAI YA LAJNA IMAILLAH YA MWAKA 2025 ITAFANYIKA TAREHE 20,21 & 22 YA MWEZI JUNI KATIKA ENEO LETU LA KITONGA JIJINI DAR ES SALAAM.

KILA MWANATANZIMU ANAHIMIZWA KUMALIZA MCHANGO WAKE WA IJTMAI NA KUWEKA NIA YA DHATI YA KUHUDHURIA IJTMAI HIYO PAMOJA NA KUJIANDAA KUSHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KIELIMU NA MICHEZO.

PIA WANATANZIMU WANAKUMBUSHWA KUSHIRIKI SHINDANO LA INSHA PAMOJA NA LILE LA QURAN KWA NJIA YA KUJIREKODI AMBAPO MWISHO WA KUTUMA INSHA NA AUDIO HIZO ZA QURAN KWA WASHIRIKI WOTE NI TAREHE 29/02/2025.

PIA WAJUMBE WOTE WA SHURA KUTOKA MATAWI MBALIMBALI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA SHURA YA KITAIFA ITAKAYOFANYIKA SIKU YA JUMAPILI YA MWEZI JUNI.

WASALAAM.

MATUMAINI YA AMANI DUNIANI

Wapendwa, Wana Majlis Ansarullah – Tanzania

Assalaam Alaikum Warahmatullah Wabarakaatuh.

Nimeombwa kutuma ujumbe kwa mnasaba wa Ijtimai yenu ya



Kitaifa. Napenda nichukue fursa hii kuwakumbusheni mambo muhimu ambayo nyinyi Majlis Ansarullah mnayo nafasi ya kipekee kuyatekeleza. Ni nyinyi ambayo mmejaliwa kufika umri wa utu uzima na hivyo wajibu wenu ni mkubwa sana wa kuwalea sio tu kizazi hiki bali na hicho kijacho. Katika ulimwengu wa leo ambao kila aina ya uhuru inapigiwa upatu chini ya kivuli cha maendeleo, wajibu wa Majlis Ansarullah umekuwa kwa mapana na marefu. Lazima mjenge mazingira ya mapenzi na maelewano katika nyumba zenu. Nyumba ndio chimbuko, hatua ya kwanza ambayo ujumbe wa Amani unaanza na kuenea. Hivyo suala la kuwatendea kwa wema wake zenu na watoto ni jambo lenye umuhimu mkubwa sana.

Inasikitisha sana kuelewa kuwa katika baadhi ya nyumba magomvi yanaibuka kutokana na vitu vidogo ambavyo havina maana hata kidogo.
Kuhusu kuwalea watoto bilkhususi katika ulimwengu huu uliochafuka sana, naweka mkazo mkubwa sana watoto kuwapatia elimu ya kidini. Waombeeni watoto wenu na waelezeni kwa upole na mapenzi. Jiepusheni na kuwakemea mara kwa mara, kwani hii inaacha athari hasi kwa watoto.

Nimeona ya kwamba pale ambapo wazazi wamejenga mazingira ya upendo na ukarimu watoto wanaendelea kushikamana na Imani, kinyume cha hivyo nyumba ambazo kuna mizozo na kutoelewana basi watoto hukimbilia kwenye dunia ambayo imekuwa na athari mbaya kwao. Huu ni mwenendo hatari. Ni vizuri kuepukana nao.
Hivyo toeni kipaumbele katika kusoma Qur'an Tukufu na kutekeleza mafundisho yake. Ushindi wetu utapatikana katika ufuata mafundisho ya Qur'an Tukufu. Hatuna silaha zozote za kidunia za kulazimisha nyoyo zitufuate. Silaya yetu pekee ni kumsujudia Allah ili Atulinde sisi, kizazi chetu na vizazi vyetu vijavyo. Dumu dawamu tuwe na mfungamano na Imani huku tukipiga hatua katika Taq'wa.

Pia tuchunguze mahusiano yetu sisi kwa sisi, kama alivyotushauri Masihi Aliyeahidiwa (as), waonesheni ukarimu wale ambao ni wakarimu. Na wasamehe hao wanaokukosea. Khulka ya kusamehe ni muhimu sana. Inaonesha watu wanazozana kuhusu vitu vidogo sana na wanakataa kusameheana. Mwendo huu unamkasirisha Allah.

Hivyo Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema, kumbukeni, kwanza Tauhiid, pili onesheni mapenzi na huruma miongoni mwenu. Onesheni mifano inayong'ara ili iwe miujiza kwa wengine. Usiifanye dunia hii kuwa shabaha yako kuu. Fanya Imani kuwa shabaha yako. Dunia ni mtumishi na chombo kwa ajili ya Imani. Hivi leo mapenzi ya dunia yamewakamata binadamu kiasi hiki ya kwamba Imani imepungua sana. Nyinyi kama Ansarullah zingatieni jambo hili. Maombi yangu ni kwamba mtazitumia siku hizi za Ijitimai yenu ya kitaifa kutafakari hayo niliyoyaeleza mkiwa na nyoyo safi na kushika njia ya ucha Mungu.

Namuomba Allah Awapeni nguvu na uwezo wa kutekeleza hayo niliyoagiza.
Na Ijtimai yenu iwe na mafanikio katika Nyanja zote.

Wassalaam
Wenu
MIRZA MASROOR AHMAD
KHALIFATUL MASIH -V



TUSIYOYAJUA KUHUSU QUR'AN TUKUFU

KUHIFADHIWA KWAKE

Na Sheikh Abid Mahmood Bhati
Jamia, Morogoro



Sawa na kanuni kuhusu kuhifadhiwa kwa Qur'ani Tukufu, Qur'ani yenyewe inastahili itoe uthibitisho kuwa imehifadhiwa na Mwenyezi Mungu.

Hapa nitaanza na aya za Qur'ani tukufu kuthibitisha kuhifadhiwa kwake;
Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu katika
Sura ya 2:24

وَإِن كُنتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَى عَبْدِنَا فَأْتُواْ بِسُورَةٍ مِّن مِّثْلِهِ وَادْعُواْ شُهَدَاءكُم مِّن دُونِ اللهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia mtumishi wetu basi leteni sura iliyo mfano wa hii, na mwaite wasaidizi wenu ghairi ya Allah ikiwa mnasema kweli.

Katika aya hii Mwenyezi Mungu anawaeleza wazi kwamba ikiwa mna shaka kuhusu yaliyomo ndani ya Qur'ani Tukufu basi watu hao wanaweza wakaitana na kusaidiana kuleta mfano wa hii Qur'ani. Wale wanaodhani wana uwezo na elimu walete mfano wa hii Qur'ani na ikumbukwe kuwa ikiwa wana shaka kwamba imetungwa basi na wao wamepewa nafasi ya kufanya kazi kama hiyo na washirikiane na kila mmoja atoe aya yake kwa sababu ikumbukwe ya kuwa umoja ni nguvu, wanaweza kutoa bora zaidi lakini kama imetoka kwa Allah basi, hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo, tena Mwenyezi Mungu akikanusha kauli yao anasema;
(b) Katika sura ya 2:25 Mwenyezi Mungu anasema kwamba

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُواْ وَلَن تَفْعَلُواْ فَاتَّقُواْ النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ

Lakini kama hamtafanya na hamtafanya kamwe basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe ulioandaliwa makafiri. (2:25)

Sawa na kauli ya Allah mpaka leo hii hakuna mtu hata mmoja, aliyefanikiwa kutoa mfano wa Qur'ani hii hata awe msomi kiasi gani ndipo tunaposema kazi ya Allah, haina kasoro na hakuna wa kushindana na Mwenyezi Mungu katika kazi zake. Na Mwenyezi Mungu anawaambia kwamba waogope moto kwa sababu hawawezi hata kidogo kuleta mfano hata wa aya kumi .
Mwenyezi Mungu anaendelea kusema katika sura ya 15:10 kuwa

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ

Hakika sisi tumeyateremsha mawaidha haya na hakika sisi ndio tuyalindao. (15:10)
Kwa hivyo; kitabu hiki Mwenyezi Mungu mwenyewe anasema kuwa yeye ndiye aliyekiteremsha na yeye ndiye mwenye jukumu la kukilinda kitabu hiki na yote yaliyomo, kwa maana hiyo kwa vile Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye mlinzi wa kitabu hiki hakiwezi kuharibiwa hata kidogo. Qur'an Tukufu ni kitabu kilichohifadhiwa kabisa kisicho na mabadiliko, nyongeza wala mapungufu kama wanavyokiri maadui wa uislam kuwa na ahadi ya Allah ya kuwa Qur'an Tukufu italindwa imethibitika.
Aya inayofuata ni kutoka sura ya 4:83 Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema

أَفَلاَ يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ اللهِ لَوَجَدُواْ فِيهِ اخْتِلاَفًا كَثِيرًا

Je? Hawaitafakari Qur'an? na kama ingalitoka kwa asiyekuwa Allah bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi (4:83)
Katika aya hii Mwenyezi Mungu ameanza kwa kuwauliza je? hawaitafakari Qur'ani, kwa maana hii kwa kutumia tu uwezo wa akili watakiri kuwa hiki ni kitabu cha Allah na kimetoka kwake.na mbele anaendelea kusema kama isingetoka kwa Allah Wangekuta hitilafu nyingi sana ndani yake . Lakini tunapotazama Qur'an Tukufu kuanzia mwanzo hadi mwisho huwezi kukuta hitilafu au kugongana kwa aya nyingine yoyote. Hiyo inadhihirisha ufasaha wa Qur'an Tukufu yaani Qur'ani itabaki safi hadi siku ya kiyama, kwa sababu ipo katika ulinzi wa Allah na neno hitilafu linaweza kuwa na maana mbili

1. Kuhitilafiana maneno ya Qur'ani Tukufu na mafundisho yaliyomo ndani yake.

2. Kuhitilafiana kwa bishara za Qur'an Tukufu na kutimizwa kwao, kwa maana hiyo Qur'ani Tukufu haina hitilafu katika maana zote hizi, na mafundisho yote yanapatana kabisa kuna baadhi ya watu wanadhani kuwa kuna aya zenye kuhitilafiana na zilizo Naasikh na Mansuukh ni kwa sababu hawakuifikiria Qur'an Tukufu kiasi cha kutosha. Kama asemavyo Allah; je? Hawaitafakari Qur'an Tukufu kitabu kinachosemwa ni cha Mwenyezi Mungu kiwe na habari zinazohitilafiana na kupinzana hicho hakiwezi kuwa kitabu cha Mwenyezi Mungu maana haiwezekani Allah alete sheria zinazotakiwa zifanye kazi wakati wote kisha zipingane.
Mwenyezi mungu anaendelelea kusema katika sura ya 87:7 kwamba

سَنُقْرِؤُكَ فَلَا تَنسَى

Hivi karibuni tutakusomesha wala hutasahau. (87:7)
Kulingana na aya hii Mwenyezi Mungu anatoa ahadi kwa kumwambia Mtume Muhammad (s.a.w) Kwamba sisi tutakusomesha wala hutaweza kusahau kamwe, yaani kuhusu masuala ya dini na mafundisho yake baada ya kufundishwa hatasahau. na tunaona baada ya Mtume Muhammad (s.a.w) kufundishwa yeye alikuwa mtu wa kwanza kutekeleza amri na hukumu zake bila kusahau hata nukta moja.
Na katika sura ya 52:3 Mwenyezi Mungu anasema

وَكِتَابٍ مَّسْطُورٍ

Na kwa kitabu kilichoandikwa. (52:3)
Hapa tunaona kitabu hiki yaani, Qur'an Tukufu Mweneyezi Mungu anadhihirisha kuwa kitabu hiki kimeandikwa. kwa hivyo hakiwezi kufutwa na yeyote kwa sababu Allah ndiye mlinzi wake na kitabaki katika usalama wake daima dawamu.

Katika sura ya 11:14-15 Mwenyezi Mungu anasema kwamba.

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ قُلْ فَأْتُواْ بِعَشْرِ سُوَرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرَيَاتٍ وَادْعُواْ مَنِ اسْتَطَعْتُم مِّن دُونِ اللهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ
فَإِن لَّمْ يَسْتَجِيبُواْ لَكُمْ فَاعْلَمُواْ أَنَّمَا أُنزِلَ بِعِلْمِ اللهِ وَأَن لاَّ إِلَـهَ إِلاَّ هُوَ فَهَلْ أَنتُم مُّسْلِمُونَ

Je, Wanasema, amekitunga? Sema: Basi leteni sura kumi zilizotungwa mfano wa hii, na waiteni wasaidizi wenu badala ya Allah ikiwa mu wakweli. Na kama wasipo waitikieni, basi jueni ya kwamba kimeteremshwa kwa elimu ya Allah, na ya kwamba hakuna aabudiwaye ila yeye tu. Basi je, mtakuwa wanyenyekevu? (11:14-15)
Na pia Mwenyezi Mungu anasema katika sura ya 41:42

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالذِّكْرِ لَمَّا جَاءهُمْ وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ

Kwa hakika wale wanaoukataa ukumbusho uwafikiapo na huo ni kitabu kiheshimiwacho. (41:42)

Katika sura ya 75:17-19 Allah anasema

لَا تُحَرِّكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ فَإِذَا قَرَأْنَاهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ

Usiutikisie ufunuo ulimi wako kwa kuufanyia haraka ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha hivyo tutakapousoma basi fuata kusomwa kwake. (75:17-19)
Katika aya hizi tunaona ya kwamba Allah anamuahidi Mtume Muhammad (s.a.w) ya kwamba kazi ya kukusanya Qur'ani Tukufu ni juu yetu, na kuusomesha na anamwambia afuate kusomwa kwake, pia Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa na hamu sana ya kuyakumbuka maneno ya wahyi kwa hivyo Allah akamtuliza kwa kuchukua jukumu hilo la kusomwa kwake. Itaendelea toleo lijalo

UANDISHI WA KURANI NA KUONYESHA JINSI KURANI ILIVYOHIFADHIWA

Kwa kuwa Qur'ani haikuteremshwa yote mara moja bali aya zake mbalimbali ziliteremshwa kidogo kidogo kwa mujibu wa haja, mazingira na wakati. Allah amehifadhi Qur'an Tukufu dhidi ya maandiko mengine matakatifu kwa uhifadhi wake ulifanywa zaidi kwa kumbukumbu zaidi kuliko kwa kalamu na karatasi kwa mujibu wa sahihi muslim; Allah alimuhakikishia Mtume s.a.w "Nitakufunulia kitabu ambacho hakiwezi kufutwa kwa maji".
Maana yake ni kuwa vitabu vingine vitatoweka kuondokana na majanga ya kidunia kama ilivyotokea kwa Taurati, Injili na maandiko mengine matakatifu. Lakini Qur'an Tukufu itahifadhiwa kwenye mioyo ya watu kiasi cha kuondoa hatari ya kupotea kwake kwa hiyo mkazo mkubwa uliwekwa katika kuhifadhi

Ukurasa wa 08

Bustani ya Washairi

MUDA
Muda nimeupoteza, kwa kuisaka dunia
Bileshi kujiumiza, kwa kila yangu hatua
Sikuweza yatimiza, yale nilokusudia
Wangapi wameipata, wale waloitafuta?

Wangapi ebu eleza, wangapi unawajua?
Dunia kuwatukuza, kuwapatia ulua
Na vingine vya nyongeza. Wakawa wametulia
Ni ipi hiyo bahari, yenye shwari za abadi?

Basi ninakuhimiza, Rai hino zingatia
Umtafute Muweza, Muumba wetu Jalia
Utaona Miujiza, akiliyo kutulia
Ukimpata Muumba, Umepata kila kitu.

Mahmood Hamsin Mubiru(wa Mamba)
Masjid Salaam
Ijumaa-01/11/2024
08:42

HAPA FYU TUNAPITA-KUMBE NYUMBANI AKHERA
Naomba nisisahau, Dunia ina mapambo
Imepambwa kinahau, mambo kuyapa maumbo
Ukiivamia kiu, haishibishi matumbo
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Si lolote si chochote, hapa sisi si wakazi
Nawapasheni utete, jambo hili mmaizi
Sisi wakati wowote, tutaondoka azizi
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Yu wapi swahiba wangu, Fadhil bin Mshamu
Inayatu ndugu yangu, Nakuchima muadhamu?
Wameenda wangu wangu, bado wangali makamu!
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Dunia kwetu ni shule, na kifo ni mapitio
Ya kwenda nyumbani kule, Akhera kwenye mafao
Njia ya sisi na wale, sote njia hiyo hiyo
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Kama walihamanika, makosa wakakusanyo
Twakuomba Ya Rabuka, punguza Uwape mwanyo
Kwa hurumayo funika, ghufiri waliyofanyo
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Yaillahi masikini, siku yangu nami hiyo
Haipo mbali lakini, kama si kesho ni leo
Nina masurufu gani, niokoke kiumbeo
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Rabi mpungufu mie, madhambi yamepandana
Mungu Nighufiri mie, Ah unisamehe sana
Peponi nikaingie, pamwe na waswalihina
Hapa fyu tunapita, kumbe Nyumbani Akhera.

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile Mbagala Rangitatu
Dar es Salaam

SEKUNDE
Na sekunde ikipita, katu huipati tena
Na kujengeka ukuta, kamwe hamtaonana
Wabaki nyuma kujuta, na la kufanya hauna
Basi isipite hivi, Sekunde moja ni mali.

Mahmood Hamsin Mubiru(wa mamba
Kiwalani-Migombani

Shairi hili liliandikwa kuwa nasaha kwa mhitimu wa Chuo Kikuu, Bi Situmai Machombe na likasomwa siku ya mahafali yake.

Yaa Rabbanaa Yaa Hadii, Mola Ulotakasika
Ulo chanzo cha uhai, mbele yako twaanguka
Yaa Ilahi Yaa Samii, kwa unyonge twatamka
Ewe Mwenye Mibaraka, Mbariki Situmai

Mbariki Situmai, Awe bingwa daktari
Mkinge na majidai, khulka ziwe nzuri
Afaidishe jamii, kwa wingi wa umahiri
Ewe mwenye kusitiri, Msitiri Situmai

Msitiri Situmai, asibaki mwenye dhiki
Ikubali dua hii, umpe mwema rafiki
Rafiki alo walii, si mwepesi kuhamaki
Ewe Uliye Razzaki, Mruzuku Situmai

Mruzuku Situmai, ashikalo linawiri
Awe mwenye kukinai, aso na moyo fakiri
Mfanye awe mtii, umlinde na kiburi
Ewe Mwenye kughufiri, Mghufiri Situmai

Mghufiri Situmai, kwa mema yako malezi
Asitupe baibui, ajali yake mavazi
Umwepushe ulaghai, hasa mahali pa kazi
Ewe Mpandisha ngazi, Mpandishe Situmai

Mpandishe Situmai, ashike vyema nidhamu
Isijefika hafai, kuyabeba majukumu
Fani za X-rei, awe mkuu mwalimu
Ewe mwenye kukirimu, Mkirimu Situmai

Mkirimu Situmai, umpe njema tabia
Mfanye mwenye khushui, katika kuhudumia
Asikose jitimai, kila inapofikia
Ewe Muongoza njia, Muongoze Situmai

Muongoze Situmai, ikuze yake elimu
Wagonjwa walio hoi, aweze kuwahudumu
Hata walio zirai, zirudi zao fahamu
Ewe mtoa Elimu, Mwelimishe Situmai

Mwelimishe Situmai, ujuzi wa makarama
Asiache dua hii, bali aombe daima
Mola uipe rifai, Rabbi zidnii 'ilma
Ewe mkuzaji mwema, Umkuze Situmai

Umkuze Situmai, wewe Akutegemee
Watu asiombe chai, bali Akushukurie
Penye hila za jinai, shari umuepushie
Ewe Mlinzi pekee, Umlinde Situmai
Sh. Ame

Usimfanyie mwenza, kwako linalokukera

Maisha nipande mbili, kichwa mwenge Cha sarafu
Tamaa sikushamiri, ukafanya badhirifu
Nafsiyo ukaijali, wenzo kosesha nafuu
Usimfanyie mwenza, kwako linalokukera

Kibaya upake rangi, rangi takayo vutiya
Uibadili konyagi, iwe maziwa na dawa
Na Usiwe mvurugi, lipa wema siubaya
Usimfanyie mwenza, kwako linalokukera

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

SAFARI TUHARAKISHE

Akhi ninakuamsha, nakuamsha Answari
Answari nakupasha, kuchele alfajiri
Sasa kujitayarisha, kuianzisha safari
Ni ndefu yetu safari, yabidi kuwakumbusha.

Safari yetu ni ndefu, mwendo wetu wa nadhari
Twende kwa uangalifu, kwa mnyoko wa suduri
Nyoyoni tuwe na khofu, kumukhofia Qahari
Mwendo wetu wa Nadhari, tukimukhofu Raufu.

Mola Tatuunganisha, dalili zipo tayari
Njia keshatuonesha, ya kupita kwa shuwari
Sisi ni kuharakisha, si vyema kutaakhari
Si vyema kutaakhari, yabidi kuwakumbusha

Moyo wa uaminifu, unaofanya ya kheri
Unaokana machafu, unaokataa shari
Kwenye maisha nyoofu, tuishi humo bukheri
Mwendo wetu wa Nadhari, tukimukhofu Raufu.

Tunatakiwa kuosha, nyoyo zetu za ghururi
Ya mui kutofatisha, tusiwe na makufari
Tuwe watu wa kukesha, kwa kumtii satari
Ni ndefu yetu safari, yabidi kuwakumbusha

Baadae na halafu, twandikwe kwa mistari
Kwa mistari mirefu, kuwa si watu hatari
Tuwe wema waongofu, tusiwe watu wa nari
Mwendo wetu wa Nadhari, tunamuomba Raufu

Tamati ninafupisha, yatosha kwa kukariri
Mola wetu Unatosha, kupandikiza athari
La haula la hasha, tunasalimu amri
Mwendo wetu wa Nadhari, nani atayekanusha?

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile Mbagala Rangitatu
Dar es Salaam

Rizika Kwa upatacho

SI Kila ukipendacho, lazima kije kwako
Rizika Kwa upatacho, hiyo ndiyo haki Yako
Usikitake kisicho, ukakivutia kwako
Utakijutia hicho, kwahizo tamaa zako

Masihi Omary stambuli kisagwa

Nipeni ujasiri

Nipeni ujasiri, wahenga mlopitia
Mwawezaje kuhimili, Wana wanapougua
Ni maumivu makali, kivipi munatulia
Mola wape utulivu, wazazi wanaumia

Tatizo linapojiri, mwana likamsumbua
Mzaziwe hatulii, kijaribu liondoa
Kulibeba hatojali, mwana kumsaidia
Mola wape utulivu, wazazi wanaumia

Mtunzi
Masihi Omary stambuli kisagwa

Hadithi ya Hamasa ya Watoto:

Misumari

Katika kijiji kidogo, mvulana wa miaka kumi aliishi na wazazi wake. Kijana huyu alikuwa na tabia mbaya.



Angekasirika kwa urahisi sana na mara nyingi alirusha hasira. Alidhihaki marafiki zake, majirani, watoto wadogo na hata wageni kwa maneno yake ya kuumiza. Jambo hili liliwahuzunisha sana wazazi wake.

Alipozungumza, wakati fulani alisahau kudhibiti hasira yake na kuchagua maneno yasiyo sahihi. Alipochukia jambo fulani, hangeacha maoni yake makali. Zaidi na zaidi ya marafiki zake na majirani walianza kumkwepa.



Wazazi wake walianza kutambua hili na walijaribu kumshauri mara kwa mara. Kwa bahati mbaya, majaribio yao yote yalishindwa.

Hatimaye, baba wa mvulana huyo alikuja na wazo. Siku moja, baba yake alimpa begi kubwa la misumari.



Alimwomba mwanawe apige msumari mmoja kwenye uzio kila mara alipokasirika au wakati wowote aliposhindwa kujizuia. Mvulana huyo aliona ni jambo la kufurahisha lakini aliamua kufuata maagizo ya baba yake hata hivyo. Kwa hiyo, hapo alikuwa. Kukimbilia kwenye uzio wa nyuma ya nyumba na kugonga msumari kila wakati alipokosa hasira.



Hasira yake ilimfanya apige misumari 30 kwenye uzio, siku ya kwanza tu! Licha ya kuwa mvulana mwenye hasira, alikuwa mtu mwenye nia na umakini, hivyo alitekeleza maagizo kwa uangalifu kila siku.




Hata hivyo, ndani ya wiki moja, idadi ya misumari iliyopigwa kwenye uzio ilipungua hadi nusu kwa sababu mvulana huyo alikuwa amechoka na ni vigumu sana kupiga misumari mara kwa mara. Alikuwa ameamua kudhibiti hasira yake badala yake kwa kuwa hilo lilikuwa rahisi zaidi.

Hatua kwa hatua, idadi ya misumari iliyopigiliwa kwenye uzio kila siku ilipungua na kupungua na hatimaye siku ikafika ambapo hakuna msumari mmoja uliopigiliwa! Ndiyo! Kijana huyo kwa kweli hakukasirika kwa siku nzima!

Siku chache zilipita. Na mvulana huyo bado aliendelea kudhibiti hasira yake. Kwa furaha, alimweleza babake jinsi ambavyo hakuwa akipigilia msumari wowote kwa kuwa hakukasirika. Baba yake bila shaka alifurahishwa sana. Sasa alimwambia mwanawe seti mpya ya maagizo. Alimwambia mvulana huyo aondoe misumari 30 mwishoni mwa kila siku ili asikasirike.

Kwa kutaka kujua, mvulana huyo alitii.



Siku kadhaa zilipita na mvulana aliweza kung'oa misumari mingi kutoka kwenye uzio, isipokuwa michache ambayo ilikuwa ngumu sana kuiondoa. Alishiriki ugunduzi huu na baba yake na wote wawili wakaenda nyuma ya nyumba.

Baba yake alimwuliza mvulana huyo, akionyesha uzio “Unaona nini, mwanangu?”

“Uzio wenye mashimo mengi ndani yake. Na kwa kucha chache ambazo haziwezi kuondolewa hata nijaribu kwa bidii kiasi gani.” akajibu.

“Ndiyo mwanangu. Unaona, misumari ni kama maneno yako mabaya, hasira ya kutisha na tabia mbaya. Walipigwa nyundo kwenye mioyo ya watu unapoumiza hisia zao. Unaweza kuondoa misumari mingi lakini mashimo na mikwaruzo kwenye uzio haiwezi kufutwa. Misumari michache hata imekwama. Hawawezi kutolewa nje kwa vile wamejipachika kwa kina sana kwenye uzio. Watabaki huko sasa kabisa. Uzio hautawahi kuonekana sawa tena.



Kwa hivyo, tunapaswa kuwa waangalifu kila wakati na kile tunachosema na kufanya kwa watu. Maneno mabaya ni kama misumari inayochoma mioyo ya watu na kuacha alama hata inapoondolewa. Baadhi ya maneno yasiyo ya fadhili kwa bahati mbaya yanaweza kuwa yakazaa sana mioyoni mwa watu. Haiwezi kufutwa. Kwa hiyo, mwanangu. Hebu tujaribu kuchagua maneno na vitendo vyetu kwa uangalifu wakati wote, insha Allah.”

Maadili:

- Kuwa mpole unaposhughulika na watu wengine
- Fikiri kabla ya kusema na kutenda
- Kudhibiti hasira yako ni hatua ambayo inaweza kufikiwa na kila mtu.

Hadith:

- “Hakika wema haupatikani katika chochote isipokuwa kukipamba, na hakiondolewi chochote isipokuwa kinakidhalilisha.” Chanzo: Sahih Muslim 2594 Daraja: Sahih "Mtu mwenye nguvu si yule anayeweza kushindana, lakini ni yule anayeweza kujizuia anapokuwa na hasira." (Bukhari)
- “Mtu mmoja akamwambia Mtume, ‘Nipe ushauri.’ Mtume, amani iwe juu yake, akasema, ‘Usikasirike. (Inayohusiana na Bukhari & Muslim)

JIFUNZE KUPIKA KISAMVU CHA NAZI

Vinavyohitajika

- Kisamvu fungu kubwa 1
- Nazi 1
- Vitunguu maji 2
- Vitunguu saumu kiasi
- Mafuta kidogo
- Chumvi kiasi

💚JINSI YA KUPIKA KISAMVU💚

1• Kichambue kisamvu,kioshe, kisha



ukitwange kilainike. Inapendeza ukikitwanga ukiwekee vitunguu saumu na pilipili kama unatumia.

2• Kichemshe mpaka kiive, kikauke

3• Bandika sufuria, weka mafuta yakipata moto weka vitunguu kaanga, kisha weka vitunguu saumu, tia mboga yetu. Weka chumvi na tui zitozito.

4. Wacha ichemke hadi tui likauke, mboga tayari.

Zingatia

Wengine hawaweki Mafuta wanaweka kila kitu baada ya kuchemsha.
Unaweza kuweka na kunde mbichi wakati unachemsha kinakuwa kitamu sana.

TUSIYOYAJUA KUHUSU QUR'AN TUKUFU

KUHIFADHIWA KWAKE

Kutoka Uk> 05

kwa moyo ili kuihifadhi na kuilinda Qur'ani Tukufu. Siku za mwanzo za Uislamu, mwanzoni wahyi ulipomshukia Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa akirudia yale maneno ili aweze kuhifadhi vizuri. kwa maana hiyo; Mwenyezi Mungu alimwambia usiutikisie huu wahyi ulimi wako kwa kuufanyia haraka hakika ni juu yetu, kuukusanya na kuusomesha. Aya ilimuhakikishia Mtume Muhammad (s.a.w) yaani hakuhitaji kurudia maneno yale haraka wakati ule wa ufunuo wenyewe kwa sababu Allah mwenyewe atamjaalia kumbukumbu ya kutosahau wahyi baada ya kuusikia mara moja wakati wa kushuka, na hivi ndivyo ilivyotokea aya zilihifadhika kwenye kumbukumbu zake Mtume Muhammad (s.a.w) mara tu baada ya kufunuliwa. Kwahiyo moyo wa Mtume Muhammad (s.a.w) mwenyewe ulikuwa mahali salama kabisa pa kuhifadhia Qur'an Tukufu . Ambapo hapakuwa na hata chembe ya zao ili pasiwepo mkanganyiko (Manahilul irfaan).

Pamoja na hayo Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa akirudia Qur'an Tukufu kwa kuisoma mbele ya Malaika Gibril (a.s_ katika mwezi wa Ramadhani kila mwaka na katika mwaka aliofariki dunia hivyo, yaani Malaika Gibril alimsomesha mara mbili {Sahih bukhar fathul baari juz 9 uk.36}

Zaidi ya hayo hakuwafundisha tu masahaba r.a maana ya Qur'an Tukufu bali aliwafanya wahifadhi maneno yake. Pia masahaba wenyewe walikuwa na ghera ya kuhifadhi Qur'an Tukufu na kila mmoja alitaka kumshinda mwenzie.

Walikuwepo wanawake ambao hawakutaka kitu kingine kama mahari kutoka kwa waume zao isipokuwa walitaka kufundishwa Qur'an Tukufu mamia ya maswahaba wakijitenga na mambo yote ya kidunia, walijitolea maisha yao kwa lengo hilo sio tu walihifadhi, bali pia walisoma wakati wa swala zao za usiku .

Sayyidna Ubaada bin Samit (r.a) alieleza kuwa kila mmoja alipohamia madina kutoka Makka Mtume Muhammad (s.a.w) alimkabidhi Ansar mmoja ili amfundishe Qur'an Tukufu mgeni. Kelele nyingi zilikuwepo ndani ya Masjid Nabawi. Kwa sauti za wasomaji na walimu wa Qur'an Tukufu kiasi hiki kwamba Mtume Muhammad (s.a.w) aliwambia washushe sauti (Maahilul irfaan juz1 uk4.}

Hadithi zinaeleza kuwa mmoja wa kundi hilo ni pamoja na Sayyidna Abu bakar (r.a), Sayyidna Umar (r.a) Sayyidna Uthman (r.a) , Sayyidna Ally (r.a) Sayyidna Talha (r.a) Sayyidna Saad, Abdullah bin Masoud (r.a) Hudhaifa bin Yaman, Salim Mawla, Abi Hudhaifa, Abu Huraira, Abdullah bin Zubair, Abdullah bin Saiib, Seyyidna Aisha (r.a) Seyyidna Hafsah n.k {Manaahilul Irfan juz 1 uk 4}

Kuna hadithi zinazotaja kuuwawa kwa wasomaji sabini miongoni mwa masahaba katika vita vya {biyr mauunah} na idadi sawa na hiyo ya masahaba. Haafidhul Qur'an waliuwawa mashahidi katika vita ya yamamah baada ya kifo cha Mtume Muhmmad (s.a.w) kwa hakika hesabu nyingine inatajwa masahaba ambao walikuwa ni mashahidi katika vita hiyo ilikuwa ni wasomaji mia saba {Umdatul qaari juz 1 uk 16-17 damascus}.

Ukweli huu unahusu Masahaba waliohifadhi Qur'an Tukufu yote katika nyoyo zao. Ama waliohifadhi sehemu tofauti za Qur'an Tukufu walikuwa hawahesabiki.

Kwa muhtasari uhifadhi wa Qur'an Tukufu katika siku za mwanzo za uislamu kwa kuhifadhi kwa moyo ilikuwa njia ya usalama na kuaminika. kwa hali ilivyokuwa wakati ule, kwa sababu idadi ya waliojua kusoma na kuandika ilikuwa ndogo na mitambo ya uchapishaji na nyingine ya utangazaji hazikufahamika. Kwahiyo kama walitegemea kalamu na karatasi wasingekuwa na usambazaji wa kutosha wala uhifadhi wa kuaminika, usingewezekana badala yake Allah amewaruzuku watu wa uarabuni kumbukumbu ya ajabu. Kiasi hiki kwamba wengi wao walikuwa na maelfu ya muungano kwenye ncha ya vidole vyao watu wa kawaida walikumbuka nasaba za koo zao. Kwahiyo nguvu ya kumbukumbu ilitumika kwa kuhifadhi Qur'an Tukufu na ilikuwa kwa kupitia njia hii kuwa aya na sura za Qur'an Tukufu zilifika kila pembe ya Arabia.

Kwa mwendelezo wa Makala hii piga simu au WhatsApp +255 658 971 662

MATUKIO KATIKA PICHA





Matukio katika Ijtimaa ya Ansarullah ya Ansarullah, Iliyofanyika katika viwanja vya Ahmadiyyaa Kitonga 06-08/Disemba/2024









Pichani baadhi ya matukio kufuatia Jalsa ya mwaka, mkoani Morogoro



Picha ya pamoja na Amir Sahib mara baada ya Jalsa ya mjini Unguja-Zanzibar (Tawi la Maungani)

Maswali kutoka katika kitabu cha

MHISANI KWA UBINADAMU

Imetayarishwa na.
Sheikh Ali Dino Tahir - Simiyu

Uk. 53

60. Mtume Muhammad SAW akiwa ana umri wa miaka 25 akamuowa bi Khadija aliyekuwa na miaka 40. baada ya kuolewa bi Khadija RA alifanyaje juu ya mali yake Jb. Bi Khadija RA alimpatia mali yake yote na watumwa wake wote kwa hiyari yake mwenyewe na kusema hiyo yote ni mali yako wewe.

61. Mtume Muhammad SAW alifanyaje juu ya mali zile alizozipata kutoka kwa mkewe Bi.Khadija RA.?
Jb. Mtume alizigawa kwa masikini mali zote na kuwaachia watumwa huru

Uk. 54

62. Wakati Mtume alipodai utume watu wa kawaida na watumwa wangapi walikuwa wanaishi mjini Makka
Jb. Watu 10000, hadi 12000. Na watumwa 500 hadi 600

63. Masahaba 50 waliomuamini mwanzoni, miongoni mwao watumwa walikuwa 35, kwanini watumwa wengi walimuamini kuliko wengine.
Jb. Kwa sabbau Mtume alikuwa mwokozi wao na alikuwa anajali sana wasiojiweza.

Uk. 55

64. Hadhrat Khabab bin Arat Radhiallah anhu aliyekuwa mtumwa akifanya kazi ya kufua chuma (mhunzi). Watu wa Makka walimuadhibu sana, utusimulie kisa chake.
Jb. Makafiri walikuwa wanauchukua mkaa wake uliokuwa ukiwaka na kumlaza juu yake na huku wakiweka juu yake mawe ili asiweze hata kukisogeza kiuno. Watu aliokuwa akiwadai fedha za utumishi wake wakakataa kumlipa. Lakini juu ya kupata hasara hizo za mali na nafsi, hakutetereka hata dakika moja bali akawa imara katika imani yake. Alama za makovu yaliyokuwa mgongoni mwake yalibakia hadi mwisho wa uhai wake. Katika utawala wa Hadhrat Umar RA alieleza masaibu(Changamoto) yaliyomkuta hapo awali.Hadhrat Umar RA akamuomba auonyeshe mgongo wake. Alipoiondoa nguo kuonyesha mgongo wake, basi mgongo mzima yalionekana meupe yaliyofanana na madoa ya mwenye ukoma. Sasa tafakarini kama Muhammad saw angekuwa amekuja kustawisha utumwa, basi ilipaswa Khabaab aje kumkata kichwa, sio alale juu ya makaa ya moto kwa ajili yake.

Uk. 55,56

65. Eleza kwa ufupi Habari ya Hadhrat Zaid bin Haritha RA aliyekuwa mtumwa wa Bi Khadija RA
Jb. Wakati jamaa zake walipopata taarifa kwamba Zaid yuko Makka, basi baba yake mzazi na baba yake mdogo wakaja na kumwambia Mtume saw kwamba, "tafadhali mpe uhuru mwanangu,tuko tayari kukupa unachotaka." Mtume saw akasema mbona mimi nimeshampa uhuru kitambo sana, anaweza kwenda popote apendapo. Hapo baba yake akamwambia, "twende zetu mwanangu." Lakini Zaid akasema: "Baba Unanihurumia sana, lakini hakuna nimpendaye zaidi kuliko Muhammad saw, kwa hiyo mimi siwezi kuondoka na kumuacha yeye."
Uk.56,57

66. Nini kilikuwa kimetokea Zaid bin Haritha RA kabla ya kumfikia Mtume?
Jibu: Alitokana na kabila la Kikristo, aliyefanywa kuwa mtumwa katika vita fulani. Aliuzwa na watu kadhaa na hatimaye akaishia kwa Khadijah, ambaye baadaye alimpatia Mtume SAW pamoja na mali zake zote.

67. Kwa nini Zaid aliamua kubaki na Mtume[saw] badala ya kuondoka na baba yake?
Jibu: Zaid alikuwa amemuamini Mtume na kumpenda sana kwa sababu ya khulka zake na upendo wake

68. Nini kilichotokea kwa Bilal Radhiallahu anhu?
Jibu: Bilal alikuwa mtumwa wa Umayya bin Khalaf, adui mkubwa wa Mtume. Alimuamini Mtume katika siku za mwanzoni za utume wake. Umayya alikuwa akimtesa Bilal kwa kumlaza kwenye mchanga wenye moto na kumwambia aache imani yake.

Uk. 57

69. Bilal Radhiallahu anhu alifanya nini wakati alikuwa akiteswa?
Jibu: Bilal Radhiallahu anhu aliendelea kusema "Ahad! Ahad!" (Allah ni Mmoja!) hata baada ya kuteswa sana.

70. Kwa nini Bilal Radhiallahu anhu aliendelea kumuamini Mtume hata baada ya kuteswa na Umayya?
Jibu: Bilal Radhiallahu anhu alikuwa ameamini Mtume na alimpenda sana. Alikuwa tayari kuvumilia mateso yoyote kwa ajili yake kwa sababu Mtume s.a.w. alikuwa mtetezi mkubwa wa wanyonge hajawahi kufikirika.

71. Msimamo thabiti wa Zaid na Bilal Radhiallahu anhu na upendo wao mkubwa juu ya Mtume unatufundisha nini?
Jibu: Mambo haya yanathibitisha kwamba Mtume Muhammad SAW alikuwa mtume mkweli na mtetezi mkubwa wa watumwa na alikuwa anawapenda kama watoto wake bila ya kujali rangi wala kabila.
Uk.58,59,60

72. Bi Sumaiya Radhiallahu anha alikuwa nani?
Jibu: Bi Sumaiya Radhiallhu anha alikuwa kijakazi ambaye alimuamini Mtume Muhammad SAW

73. Abu Jahal alimfanyia nini Bi Samiyya kabla ya kumuua?
Jibu: Alimtesa sana ili amlazimishe aachane na imani yake ya Kiislam hatimae akamuua.

74. Kifo cha Bi Samiyya Radhiallhu anha kinaonyesha nini kuhusu imani yake?
Jibu: Kifo chake kinaonyesha imani yake imara na ujasiri wake.

75. Je, kuna mifano mingine ya watumwa walioteswa sana kwa ajili ya imani yao kwa Mtume Muhammad SAW ?
Jibu: Ndiyo, maandiko haya yanataja mifano mingine ya watumwa kama vile Hadhrat Ammaar ,Suhaib, Abu Fakih na Hadhrat Aamir bin Fuhayra Radhiallahu Anhum

76. Unajua nini Kuhusu Hadhrat Ammar bin Yasir Radhiallahu anhu
Hadhrat Ammar bin Yasir Radhiallahu anhu alikuwa Mtumwa na wazazi wake pia walikuwa watumwa huko Makka waliomuamini Mtume SAW mwanzoni. Abujahli aliwafunga hadharani wazazi wake na kuwapiga sana wazazi wake mbele yake ili wao na yeye waachane na Imani zao lakini wote wakawa imara hatimaye Abujahli aliwaua wazazi wake mbele yake lakini hata hivyo Hadhrat Ammar hakuacha Imani yake.Kwa ufupi Abujahli alishindwa

77. Taja majina ya wazazi wake Hadhrat Ammar bin Yasir Radhiallahu anhu
Jibu: Hadhrat Yasir Radhiallhu anhu na Hadhrat Sumaiya Radhiallahu anhuma

78. Je, unajua majina ya wanawake vijakazi walioteswa sana kwa sababu ya Imani yao lakini hawakuacha uislam.
Jibu: Hadhrat Labina, Hadhrat Zaniza,Hadhrat Nadhiya,Hadhrat Ummi Ubais na Hadhrat Hamama (Mungu awe radhi nao wote)

79. Unajua nini kuhusu Hadhrat Labina na Hadhrat Zaniza radhiallhu anhuma?
Jibu: Hawa wote wawili walikuwa watumwa vijakazi wa Hadhrat Omari RA na alikuwa anawatesa sana kwa sababu ya Imani zao wakati baado yeye hajasilimu.

80. Abujahli alimfanyia nini Hadhrat Zaniza Radhiallahu anha
Jibu: Siku moja Abujahli alimpiga mpaka alipofuka (amekuwa kipofu)

81. Abu Jahli alipokuwa akimuona Hadhrat Zaniza Radhiallah Anha alikuwa anasemaje:
Alikuwa anasema kwa hasira na dharau kwamba: Je, sisi tumekuwa wa kuchukiza kiasi hiki kwamba Zaniza ameiamini dini ya kweli na sisi tumeikosa? (Lakini yeye hakujua kwamba Islamu ni rehema na fadhili za Mwenyezi Mungu anambariki amtakaye)

82.Kwa nini Mtume Muhammad SAW alikuwa muhimu kwa watumwa?
Jibu: Mtume Muhammad alifundisha ujumbe wa usawa na haki kwa wote, bila kujali hali yao ya kijamii. Hii ilikuwa ni habari njema kwa watumwa ambao walikuwa wakinyanyaswa na kubaguliwa sana uarabuni.
Uk.61

83. Hadhrat Hamama Radhiallahu anha alikuwa nani?
Jibu: Hadhrat Hamama Radhiallahu anha alikuwa mama yake mzazi wa Hadhrat Bilal Radhillahu anhu na hawa wote walipata mateso makubwa kwa sababu ya kusilimu kwao.

84. Katika miaka saba ya mwanzo ya Islam watu wangapi walimuamini Mtume Muhammad SAW
Jibu: Watu 40 tu. (15 Watumwa na 25 watu waliokuwa huru)

85. Je, Mtume Muhammad SA alikuwa ana huruma kwa watumwa wasiokuwa waislamu?
Jibu: Mtume Muahmmad SAW alikuwa anahurumia watumwa wote bila kujali dini au rangi zao.
Uk. 61,62

86. Kulitokea nini mpaka Hadhrat Hamza RA alislimu?
Jibu: Siku moja Hadhrat Hamza alipofika nyumbani kijakazi wake alimpatia habari kwamba Abujahli alimtukana sana na kumkejeli kijana wako Muhammad saw. Lakini Muhammad hakumjibu chochote mpaka alichoka kutukana. TUKIO HILI LILIKUWA CHANZO CHA KUSILIMU KWA HADHRAT HAMZA ra.
Uk . 63

87. Mtume Muhammad SAW alipoenda kuhubiri mji wa Taif alifukuzwa na kupigwa mawe na washenzi, alijeruhiwa kiasi kwamba damu ya mwili iliganda na viatu vyake.Nje ya Taif kulikuwa Bustani alipoomba msaada.Nani alimsaidia.?
Jibu: Mtumwa mmoja aitwaye Addas alimsaidia Mtume SAW ,alipoona hali ya Mtume alijisikia vibaya sana hadi machozi yalimtoka,basi alimpa pole na kumpatia zabibu.
Uk . 64

88. Je, kulikuwa na utumwa kabla ya Mtume Muhammad (SAW)?
Jibu: Ndiyo, utumwa ulikuwepo kabla ya Mtume Muhammad (SAW) katika nchi zote duniani

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

HISTORIA YA AHMADIYYA ZANZIBAR

Kutoka uk. 12

Ni wakati wa mbashiri Mkuu Sheikh Jamil-ur - Rahman.

Mwezi Disemba mwaka huo huo 1979 nilihama Dar na kurudi Pemba. Nikiwa Pemba nilitambulishwakwanduguyangu wa imani hayati Bw. Mbwana Said ambaye alikuwa akifanya kazi Wete Kaskazini Pemba . Mimi ni mpemba wa kwanza Ahmadiya. Alhamdullilah.

6. Mtu wa sita ni Bi . Bimkubwa bint kombo wa Pemba. Alijiunga akiwa Mtwara kwenye mafunzo ya uuguzi mwaka 1984, baada ya kusoma vitabu viwili . YESU KAFIA WAPI NA SANDA YA YESU . Miongoni mwa watoto wake Abubakar Burhani yupo imara Allah amuimarishe zaidi.

7. Mtu wa saba ni Mwl Said Othman Mohd ambaye alijiunga mwaka 1989 Dar es Salaam wakati wa Mbashiri Mkuu Sheikh Bajwa. Yeye ni mwenye juhudi kwenye mahubiri, na vijana wengi wa Zanzibar wamejiunga na jumuiya kupitia mahubiri yake. Allah sw amuimarishe zaidi, amin.

8. Mtu wa nane ni Bw. Ameir Mahmoud Kheri alijiunga mwaka 1990 kupitia mahubiri ya Hayati Bw. Shaibu, Bw Ameir ni mtu wa kwanza aliyejiunga akiwa Zanzibar.

9. Mtu wa tisa ni Sheikh Abdul-Rahman Mohd Ame ambaye alijiunga mwaka 1991 Dar es Salaam. Mwaka 1996 alitoa wakfu maisha yake kutumikia dini.

10. Mtu wa kumi ni Bi Wahida bint Mahmoud Kheri. Alijiunga mwaka 1992 Zanzibar kupitia Bw. Shaibu.

11. Wa kumi na moja ni Bw. Rashid Mubarak aliyejiunga mwaka 1992 kupitia Sheikh Abdul- Rahman Ame.

12. Wa kumi na mbili ni Bw. Mohd Othman Khatib. Alijiunga mwaka 1992 kupitia Mwl. Said Othman.
13. Wa kumi na tatu ni Bw. Salum Juma Khamis. Alijiunga mwaka 1994 kupitia Mwl. Said Othman.

14. Wa kumi na nne ni Hayati Bw. Ahmada Haji Machano, mdogo wake Bw. Ame Haji aliyeishi Dar es Salaam. Bwana Ahmada alifariki mwaka 1995.

UONGOZI NA SALA YA IJUMAA

Waahmadiya wa Zanzibar walianza kusali sala ya ljumaa nyumbani kwa Hayati Bw. Said Magerwa na baadae nyumbani wa Hayati Bw. Mbwana Said Miembeni. Kwenye miaka ya 1990 walisali Migombani nyumbani kwa Mwalimu Said Othman . Viongozi wao wa awali ni Hayati Bw. Said Magera na Hayati Bw.M'bwana Said kwenye miaka ya 1980s. Ilipofika miaka ya 1990s wakaongeza nguvu vijana wapya mwl Said Othman na Sheikh Abdul-Rahman M. Ame.

Mahubiri yalipamba moto baada ya kujiunga vijana wabichi hawa Mwl Saidi Othman na Sheikh Abdul-Rahman Ame, walitumia mbinu mmoja kujifanya mpinzani. Mahojiano yao yalivuta watu kuwasikiliza na hivyo ndivyo ujumbe ulivyowafikia wasikilizaji. Mbinu hii ilifanikiwa na ilizaa matunda Alhamdullilah.

I KUKUA

Miongoni mwa matunda yaliyopatikana kwenye miaka hio 1990 ni ;-

1.Bw, Rashid Mubaraka - 1992
2. Bw Mohd Othman Khatib–1992
3. Bw Salum Juma Khamis - 1994
4. Bw Ahmada Haji Machano - 1995
5. Bw. Omar Khamis Ali - 1996
6.Bw. Abdul -Rahman Y. Ali - 1996

MAENDELEO ZAIDI

Kwenye miaka ya 2000 Jumuiya ilizidi kuimarika na waliojiunga ni kama ifuatavyo :-

1. Bwana Hassan Mussa Hassan, mwaka - 2000
2. Bwana Yussuf Othman Mohd ,mwaka -2000
3. Bi Wahida Othman Ali ,mwaka - 2001
4. Bw.Mohd Khamis Ameir (Bingo), mwaka - 2003
5. Bi Asya Mussa Hassan ,mwaka - 2006
6. Bi Fatma Hassan Ali, mwaka -2007
7. Bw Nassor Twalib Khatib ,mwaka - 2008
8. Dr. Ahmada lssa Feruzi , mwaka - 2009
9. Bi Khadija Mwalimu Mwinyi, mwaka - 2011
10. Bw. Nassir Abdalla Daud, mwaka - 2012
11. Bw. Mohd Mzee Swaleh, mwaka - 2013

12. Mwl .Mzee Mohd Mzee mwaka-2013
13. Bw. Mfaume Abdalla Saleh, mwaka - 2014

14. Bw Said Khalfan Said, mwaka -2014

15. Bi mariam Juma Ali , mwaka - 2015

16. Bi Rahma Batwana Hamad, mwaka - 2015
17. Bw. Ali Suleiman Nuru, mwaka - 2015
18. Bi Fatma Ali Ame, mwaka -2016
19. Bi Mwapili Shauri Mussa, mwaka - 2016

20. Bi Asha Mbarawa , mwaka - 2018
21. Bi Mariam Mohd Ame, mwaka -2018
22. Bw. Juma Bundala Masanja, mwaka - 2018
23. Bi Hadiya Mwichum Khamis, mwaka -2019
24. Bi Aisha Rasmi Kimario , mwaka - 2019
25. Bw Sleyum Swaleh Hassan, mwaka -2019
26. Bi Mtumwa Omar, mwaka 2020
27. Bw Abdulaziz Juma Kindy, mwaka - 2020
28. Bw, Mohd Swaleh Hassan, mwaka - 2020
29. Bi Amina Mohd - Ni mzanzibari aliyejiunga Dar es Salaam mwaka 1996 kwa sasa anaishi Zanzibar.

Ndani ya kipindi hiki kuna Waahmadiya kutoka Tanzania bara wanaishi Zanzibar.

1.Bw Salum Khamis Mbambwa - Mzawa
2. Bw Kheri Rashid Maovera
3.Bw Hashim Rashid Maovera

Tunao pia vijana waliozaliwa katika jumuiya

1. Bw Said Mbwana Said
2. Bw Othman Said Othman
3. Bw Juma Said Othman
4. Bw Abuubakar Burhan Mohd
5. Bi Sabra Said Mohd
6. Bi Maryam Mussa Hassan
7. Bi Bushra Bashir Mbalawa
8. Bi Talhata Said Mbwana
9. Bw Ya'qub Ameir Mahmoud
10. Bi Aisha Ameir Mahmoud
11. Bi Salwa Omar Khamis
12. Bi Fatma Omar Khamis
13. Bi Fatma Salum Juma
14. Bi Warda Salum Juma
15. Bw Juma Salum Juma
16 Bw Said Salum Juma

Kuna Wazanzibari wanaoishi Tanzania bara

1. Hayati Bw Ame Haji Machano
2. Bw Ahmad Ame Haji
3. Bw Juma Ame Haji
4. Shekh Abdul-Rahman M. Ame
5. ZafrulahAbdul-Rahman Mohd
6. Fadhlullah Abdul-rahman Mohd
7.Nasrullah Masruur Abdul-Rahman
8.Bw Makame Mgaya Adam
9. Bi Fatma Shaib Kondo
10. Bw Hussein Omar Rawa
11. Mwl. Ali Swaleh Hassan
12. Mwl. Mzee Mohd Mzee

JADWELI LA WANAJAMATI WA ZANZIBAR HADI JUNE 2024

MATAWI	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
MIGOMBANI			
Wakubwa	14	10	24
Watoto	10	10	20
JUMLA	24	20	44
MAUNGANI			
Wakubwa	15	13	28
Watoto	22	11	33
JUMLA	37	24	61
UNGUJA UKUU			
Wakubwa	06	09	15
Watoto	10	10	20
JUMLA	16	19	35
JUMLA KUU			
Wakubwa	35	32	67
Watoto	42	31	73
JUMLA	**77**	**63**	**140**

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah

UK. 03






<<<Tanzia>>>

Tukiwa mtamboni tunapokea taarifa ya msiba wa Mzee Salum D. Mtamila. Maelezo zaidi toleo lijalo.

Innalillahi wa innailaihi raji'un

HISTORIA YA AHMADIYYA ZANZIBAR

Kutoka toleo lililopita




WAAHMADIYA WA AWALI ZANZIBAR

Waahmadiya wa mwanzo ni wale waliotokea Tanzania bara na kwenda kuishi Zanzibar nao ni :

1.Hayati Bw, Omar Rawa aliyetokea Tanga na kwenda kuishi Zanzibar kwa shughuli zake za ujenzi. Yeye alifika Zanzibar wakati wa utawala wa Sultani Khalifa bin Haroub (1911 -1960) akiwa tayari ni Ahmadiya. Alifariki na kuzikwa Zanzibar mwaka 1998. Allah amrehemu. katika watoto wake Husein ndio yuko imara katika Jamaat Allah amuimarishe zaidi na anaishi Tanzania bara.

2. Wa pili ni Hayati Bw. Said Megerwa mwenyeji wa Rufiji. yeye alifika Zanzibar kwenye miaka ya 1970° akiwa Meneja wa Benki kuu tawi la Zanzibar. Akiwa tayari ni Ahmadiyya . Alifariki na kuzikwa mwaka 1997 Zanzibar. Allah amrehemu


3. Mtu wa tatu ni hayati Bw. Mbwana Said. Alifika Zanzibar kipindi cha Sultani Khalifa bin Haroub akiwa na umri wa miaka 13. Ni vigumu kujua mwaka aliojiunga ila ni zamani sana yamkini kwenye miaka ya 1960s. Alikuwa mtumishi wa Serikali na alishi Zanzibar muda wote. Alifariki na kuzikwa Zanzibar mwaka 1999. Miongoni mwa watoto wake ni Bw. Said Mbwana Said yuko imara. Allah amuimarishe zaidi MILANGO YAFUNGUKA



4. Mtu wa nne kujiunga ni Hayati Bw. Shaib Kondo Haji mzaliwa wa Zanzibar mwaka 1977. Ni mzanzibari wa kwanza Ahmadiya alieishi Zanzibar (wa kwanza kabisa ni Bw . Ame Haji Machano aliyeishi Dar-es-salaam) alifariki tarehe 25May 2019 Zanzibar. Katika watoto wake, Bi Fatma Shaib ndiye yuko imara . Allah azidi kumuimarisha.

5. Watano ni mimi mwandishi wa makala hii Aliy Khamis Juma. Nilijiunga nikiwa naishi Dar es Salaam tarehe 12 July 1979 baada ya maonyesho ya saba saba. Mimi ni zao la maonyesho ya saba saba (1979).

HABARI UK> 11



SANATAN DHARM

(Swahili Translation)

Sanatan Dharm is a short essay written by the Promised Messiah[as] in 1903. It addresses the controversial Āryah Samāj tenet of Niyoga.

In this vivid analysis the author persuasively argues that Niyoga is, in its essential features, at complete variance with human dignity, honour and all universally accepted norms of morality.

ISBN 1848805446

SANATAN DHARM

(Dhehebu la dini ya Kibaniani)

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Je, Wajua?

Jonny Kim ni Luteni Kamanda wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, aliyekuwa Navy SEAL, daktari (M.D. kutoka Shule ya Matibabu ya Harvard), naval aviator, na astronaut wa NASA.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,000/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com